

SHERIA YA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI

Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007 in Ibara 68 zilizogawanyika katika Sehemu tisa kama ifuatavyo:-

Sehemu ya I ni utangulizi inayohusisha jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika.

Sehemu ya II ni misingi na malengo makuu ya sera yaliyotengwa kutekelezwa na Sheria.

Sehemu ya III yenye Ibara ya 5 mpaka 13 inahusu muundo wa utawala unaojumuiisha majukumu na mamlaka ya Waziri, Tume ya Mipango Matumizi ya Ardhi, na kuteuliwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa kuiongoza Tume. Ibara ya 8 inaweka Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi kuwa mamlaka ya kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na kushitaki mahakamani, ili kuhakikisha kuwa maagizo na maelekekezo yake yanafuatwa.

Sehemu ya IV inahusu upatikanaji wa fedha za Tume na mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni za kutoza ada. Ibara ya 14 mpaka 17.

Sehemu ya V yenye Ibara ya 18 mpaka 38 inaunda mamlaka za upangaji. Pia inaweka mchakato wa kutayarisha na kutekeleza mipango. Ibara ya 18 inaweka mamlaka za upangaji (*planning authorities*). ambazo ni Halmashauri za Vijiji, Halmashauri za Wilaya na Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ambayo ni mamlaka ya ki-Taifa ya upangaji wa matumizi ya ardhi yinayohusika kuandaa Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi, mipango ya kanda na kuratibu utayarishaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kutoka Wilaya kupitia sekretariati za mikoa.

Sehemu ya VI, Ibara ya 39 hadi ya 45 inatoa mamlaka maalum kwa mamlaka za upangaji ikiwa ni pamoja na uwezo wa kutwaa ardhi kwa makusudio ya kuipangia matumizi, kuiwekea mipaka, kuigawanya, kuipangilia upya, kufanya marekebisho, ofisa aliyeruhusiwa na Mamlaka ya Upangaji kuingia ndani ya ardhi inayokusudiwa kupangiwa matumizi, kutoa haki za matumizi ya ardhi na uhifadhi wa majengo ya kumbukumbu za kihistoria.

Sehemu ya VII inajumuisha Ibara ya 46 mpaka 61. Sehemu hii inaweka ulazima wa kuzingatia sheria hii, udhibiti na uratibu wa kazi za upangaji. Hii ikiwa ni pamoja na utwaji ardhi wa lazima kwa kuzingatia mipango iliyoidhinishwa pamoja na madaraka ya mamlaka za upangaji katika kudhibiti matumizi ya ardhi. Sehemu hii pia inampa uwezo Waziri kwa kuwasiliana na Mawaziri wengine wanaohusika kuweka mfumo ambao unaweza kutumiwa na mamlaka za upangaji wa kutoa motisha kwa watekelezaji wa mipango kwa hiari. Sehemu hii pia inatoa uwezo kwa Mamlaka za Upangaji kutoa ilani ya kuzuia uendelezaji unaofanywa kinyume na mpango. Aidha inatoa nafasi ya rufaa kwa mtu anayeona kuathiriwa na ilani ya aina hiyo. Ibara ya 51 inampa Mkurugenzi Mkuu madaraka ya kumteua ofisa au mkaguzi wa kuendesha mashtaka ambaye kwa idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka ataendesha mashtaka yote dhidi ya kosa lolote litakalofanywa chini ya Sheria hii.

Sehemu ya VIII, Ibara ya 62 hadi 63 inabainisha makosa, adhabu na faini kwa waendelezaji wanaovunja masharti ya mpango ulioidhinishwa.

Sehemu ya IX yenye Ibara ya 64 mpaka 68 inatoa maelezo ya jumla ikiwa ni pamoja na uwezo wa Waziri kutunga Kanuni kuhusu utoaji, urekebishaji na ufutwaji wa mpango wowote ulioidhinishwa, kanuni za kutoza ada, viwango vya upangaji, amri na maagizo mengine yoyote. Sehemu hii inawapa uwezo Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Upangaji au mtu yeyote aliyeruhusiwa kutoa ilani ya kupata taarifa kutoka kwa mtu yeyote kuhusu ardhi na maendelezo yake yanayohusika na mpango. Ibara ya 66 inafuta Sheria ya Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Sura 116 ya mwaka 1984.

Kusoma Sheria yote tembelea “*Land Policy and Regulations*” katika tovuti hii.